TANGAZO LA SERIKALI Na. 603 la Tarehe 10/10/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),

(SURA YA 288)

# NOTISI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 7(2))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUANZISHA HALMASHAURI YA MJI BAGAMOYO YA MWAKA 2025

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kuanzisha Halmashauri ya Mji Bagamoyo ya Mwaka 2025.

Taarifa

**2**. Taarifa inatolewa kwa umma kwamba baada ya muda wa Notisi hii kumalizika, eneo lililokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kama linavyoonekana katika Jedwali la Notisi hii pamoja na mipaka na maeneo yake ya kiutawala linakusudiwa kuanzishwa kuwa Halmashauri ya Mji Bagamoyo.

Maoni au pingamizi

**3**. Taasisi au mtu yeyote ambaye anaweza kuathiriwa na uamuzi wa kuipandisha hadhi ya Mji Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo anaweza kuwasilisha kwa maandishi pingamizi au maoni yake kwa njia ya barua ndani ya muda wa miezi miwili kutoka tarehe ya Notisi hii kwa anwani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
Mji wa Serikali-Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S.L.P 1923,
41185 DODOMA,
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

SEHEMU A
(Jina la Halmashauri Mpya ya Mji)

1. Halmashauri ya Mji Bagamoyo

SEHEMU B
(Jina la Halmashauri ya Wilaya iliyopo)

1. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo

SEHEMU C
(Maeneo ya kiutawala ya Halmashauri ya Wilaya inayopandishwa hadhi)

HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO

| Halmashauri | Na. | Tarafa | Na. | Kata | Na. | Kijiji | NA. | Kitongoji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Bagamoyo | 1 | Yombo | 1 | Yombo | 1 | Yombo | 1 | Chombe Juu |
| | | | | | | | 2 | Lwazi |
| | | | | | | | 3 | Ukwamani |
| | | | | | | | 4 | Goba |
| | | | | | | | 5 | Ushokolani |
| | | | | | | | 6 | Fulwe |
| | | | | | | | 7 | Yombo |
| | | | | | | | 8 | Magoza |
| | | | | | | | 9 | Masogola |
| | | | | | | | 10 | Kiegea "B" |
| | | | | | 2. | Chasimba | 11 | Miwaleni |
| | | | | | | | 12 | Mfulu |
| | | | | | | | 13 | Chasimba |
| | | | | | | | 14 | Shangweni |
| | | | | | | | 15 | Kiegea "A" |
| | | | | | | | 16 | Bwembweni |
| | | | | | 3. | Kongo | 17 | Mikuge |
| | | | | | | | 18 | Shuleni |
| | | | | | | | 19 | Nuwa (Kambini) |
| | | | | | | | 20 | Kajiungeni |
| | | | | | | | 21 | Chombe |
| | | | | | | | 22 | Kongo |
| | | | | | | | 23 | Umakondeni |
| | | | | | | | 24 | Uzaramoni |
| | | | | | | | 25 | Mzizima |
| | | | | | 4 | Matimbwa | 26 | Ngogomoni |
| | | | | | | | 27 | Kimbehengwa |
| | | | | | | | 28 | Chamkwela |
| | | | | | | | 29 | Kikuichola |
| | | | | | | | 30 | Zombengalawa |
| | | | | | | | 31 | Matimbwa |
| | | 2 | Fukayosi | | 5 | Fukayosi | 32 | Fukayosi |

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

| Halmashauri | Na. | Tarafa | Na. | Kata | Na. | Kijiji | NA. | Kitongoji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | 33 | Lusako |
| | | | | | | | 34 | Kalimeni |
| | | | | | | | 35 | Kulwi |
| | | | | | | | 36 | Umasaini |
| | | | | | | | 37 | Mtakuja "A" |
| | | | | | | | 38 | Mtakuja "B" |
| | | | | | | | 39 | Mwanavuli |
| | | | | | | | 40 | Ndoleni |
| | | | | | 6 | Mwavi | 41 | Mwavi "A" |
| | | | | | | | 42 | Mwavi "B" |
| | | | | | | | 43 | Sengasenga |
| | | | | | | | 44 | Vigwaza |
| | | | | | | | 45 | Kudibaha |
| | | | | | | | 46 | Segwa |
| | | | | | | | 47 | Zemba |
| | | | | | 7 | Kidomole | 48 | Relini |
| | | | | | | | 49 | Kinyemvuli |
| | | | | | | | 50 | Usinga |
| | | | | | | | 51 | Mwanasenga |
| | | | | | | | 52 | Vihagate |
| | | | | | 8 | Mkenge | 53 | Mgorani |
| | | | | | | | 54 | Chang'ombe |
| | | | | | | | 55 | Mkwama |
| | | | | | | | 56 | Engelo |
| | 2 | Mwambao | 3 | Zinga | | | 57 | Kwa Faki |
| | | | | | | | 58 | Bisibisi |
| | | | | | | | 59 | Kijiweni |
| | | | | | | | 60 | Bondeni |
| | | | | | | | 61 | Mbuyuni Kondo |
| | | | | | | | 62 | Kibuyuni Kondo |
| | | | | | | | 63 | Kwadosi |
| | | | | | | | 64 | Chaponda |
| | | | | | | | 65 | Mwajimbo |
| | | | | | | | 66 | Gwazo |
| | | | | | | | 67 | Gongoni Kondo |
| | | | | | | | 68 | Kigovu |
| | | | | | | | 69 | Kondo Bondeni |
| | | | | | | | 70 | Kibuyuni |
| | | | | | | | 71 | Kibuba |
| | | | | | | | 72 | Kiamboni |
| | | | | | | | 73 | Kidugu |
| | | | | | | | 74 | Kibwagogo |
| | | | | | | | 75 | Gongoni Zinga |
| | | | | | | | 76 | Dagaza |

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

| Halmashauri | Na. | Tarafa | Na. | Kata | Na. | Kijiji | NA | Kitongoji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | 77 | Maamata |
| | | | | | | | 78 | Kituli |
| | | | | | | | 79 | Chambeo |
| | | | | | | | 80 | Kokoto |
| | | | | | | | 81 | Mbuyuni |
| | | | | | | | 82 | Kiegea |
| | | | | | | | 83 | Msoka |
| | | | | | | | 84 | Mchangakichwa |
| | | | | | | | 85 | Mchangakichwa |
| | | | | | | | 86 | Changuruwe |
| | | | | | | | 87 | Mikungalungo |
| | | | 4 | Kerege | | | 88 | Kitonga |
| | | | | | | | 89 | Kwa Manofu |
| | | | | | | | 90 | Amani |
| | | | | | | | 91 | Nyakahamba |
| | | | | | | | 92 | Matumbi |
| | | | | | | | 93 | Kwakiwete |
| | | | | | | | 94 | Kilemela |
| | | | 5 | Mapinga | | | 95 | Kwa Kibosha |
| | | | | | | | 96 | Mtambani |
| | | | | | | | 97 | Kimele |
| | | | | | | | 98 | Udindivu |
| | | | | | | | 99 | Changwahela |
| | | | | | | | 100 | Kiembeni |
| | | | | | | | 101 | Tungutungu |
| | | | | | | | 102 | Kiharaka |
| | | | 6 | Kiromo | | | 103 | Kiromo "A" |
| | | | | | | | 104 | Kiromo "B" |
| | | | | | | | 105 | Mandawe |
| | | | | | | | 106 | Chagga "A" |
| | | | | | | | 107 | Chagga "B" |
| | | | | | | | 108 | Mbuyuni |
| | | | | | | | 109 | Kitonga "A" |
| | | | | | | | 110 | Kitonga "B" |
| | | | | | | | 111 | Kitopeni "A" |
| | | | | | | | 112 | Kitopeni "B" |
| | | | | | | | 113 | Migudeni |
| | | | | | | | 114 | Mto wa Nyanza |
| | | | | | | | 115 | Goba |
| | | | | | | | 116 | Magole |
| | | | | | | | 117 | Mataya Bondeni |
| | | | | | | | 118 | Baukani "A" |
| | | | | | | | 119 | Baukani "B" |
| | | | | | | | 120 | Kimeremeta |
| | | | | | | | 121 | Kivumo mataya |

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

| Halmashauri | Na. | Tarafa | Na. | Kata | Na. | Kijiji | NA. | Kitongoji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | 122 | Gongoni |
| | | | | | | | 123 | Magharibi |
| | | | | | | | 124 | Mlatange |
| | | | | | | | 125 | Vikindu |
| | | | | | | | 126 | Chanagoi |
| | | | | | | | 127 | Chambezi 'A' |
| | | | | | | | 128 | Chambezi 'B' |
| | | | | | | | 129 | Kiwangwa |
| | | | | | | | 130 | Vigonda |
| | | | 7 | Dunda | | | 131 | Dunda |
| | | | | | | | 132 | Mwambao |
| | | | | | | | 133 | Tandika |
| | | | | | | | 134 | Ramiya |
| | | | | | | | 135 | Mwanakalenge |
| | | | | | | | 136 | Majani Mapana |
| | | | | | | | 137 | Benki |
| | | | | | | | 138 | Soko Jipya |
| | | | | | | | 139 | Mangesani |
| | | | | | | | 140 | Shaurimoyo |
| | | | | | | | 141 | Kaole Ufundi |
| | | | | | | | 142 | Miti Mingi |
| | | | | | | | 143 | Bondeni |
| | | | | | | | 144 | Madukani |
| | | | | | | | 145 | Ukuni |
| | | | | | | | 146 | Mto wa Nyanza |
| | | | 8 | Magomeni | | | 147 | Maji Coast |
| | | | | | | | 148 | Bong'wa |
| | | | | | | | 149 | Magomeni "C" |
| | | | | | | | 150 | Sanzale |
| | | | 9 | Nianjema | | | 151 | Kimarang'ombe |
| | | | | | | | 152 | Magomeni "B" |
| | | | | | | | 153 | Magomeni "A" |
| | | | | | | | 154 | Nianjema "A" |
| | | | | | | | 155 | Nianjema "B" |
| | | | | | | | 156 | Nianjema "C" |
| | | | 10 | Kisutu | | | 157 | Kisutu |
| | | | | | | | 158 | Mji Mpya |
| | | | | | | | 159 | Mianzini "A" |
| | | | | | | | 160 | Mianzini "B" |
| | | | | | | | 161 | Mwembe Mkole |
| | | | 11 | Makurunge | | | 162 | Mtoni |
| | | | | | | | 163 | Mkwajuni |
| | | | | | | | 164 | Gezaulole |
| | | | | | | | 165 | Kifude |
| | | | | | | | 166 | Kitame |

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

| Halmashauri | Na. | Tarafa | Na. | Kata | Na. | Kijiji | NA. | Kitongoji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | 167 | Kibaoni |

SEHEMU D
(Maeneo ya kiutawala ya Halmashauri Mpya ya Mji)

HALMASHAURI YA MJI BAGAMOYO

| HALMASHAURI | NA | TARAFA | NA. | KATA | NA. | MTAA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Bagamoyo | 1 | Yombo | 1 | Yombo | 1 | Yombo |
| | | | | | 2 | Chasimba |
| | | | | | 3 | Kongo |
| | | | | | 4 | Matimbwa |
| | | | 2 | Fukayosi | 5 | Fukayosi |
| | | | | | 6 | Mtakuja |
| | | | | | 7 | Mwavi "A" |
| | | | | | 8 | Mwavi "B" |
| | | | | | 9 | Kidomole Kisumbi |
| | | | | | 10 | Kidomole Relini |
| | | | | | 11 | Mkenge |
| | 2 | Mwambao | 3 | Zinga | 12 | Mlingotı A |
| | | | | | 13 | Kondo |
| | | | | | 14 | Mlingoti B |
| | | | | | 15 | Hospitali |
| | | | | | 16 | Mkuza |
| | | | | | 17 | Zinga B |
| | | | | | 18 | Zinga A |
| | | | 4 | Kerege | 19 | Kitonga |
| | | | | | 20 | Amani |

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

| HALMASHAURI | NA. | TARAFA | NA. | KATA | NA. | MTAA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 21 | Matumbi |
| | | | | | 22 | Kwakiwete |
| | | | 5 | Mapinga | 23 | Kwa Kibosha |
| | | | | | 24 | Mpiji Darajani |
| | | | | | 25 | Mtambani |
| | | | | | 26 | Kimele |
| | | | | | 27 | Kiharaka |
| | | | | | 28 | Kiembeni |
| | | | | | 29 | Udindivu |
| | | | | | 30 | Changwahela |
| | | | | | 31 | Tungutungu |
| | | | 6 | Kiromo | 32 | Kiromo "A" |
| | | | | | 33 | Kiromo "B" |
| | | | | | 34 | Kitopeni |
| | | | | | 35 | Mataya "A" |
| | | | | | 36 | Mataya "B" |
| | | | | | 37 | Buma "B" |
| | | | | | 38 | Chambezi |
| | | | | | 39 | Buma "A" |
| | | | 7 | Dunda | 40 | Ramia |
| | | | | | 41 | Tandika |
| | | | | | 42 | Majani Mapana |

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

| HALMASHAURI | NA | TARAFA | NA. | KATA | NA. | MTAA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 43 | Ukuni |
| | | | | | 44 | Kaole |
| | | | 8 | Magomeni | 45 | Muungano |
| | | | | | 46 | Bomani |
| | | | | | 47 | Sanzale |
| | | | 9 | Nianjema | 48 | Nianjema "A" |
| | | | | | 49 | Magomeni Sokoni |
| | | | | | 50 | Nianjema "C" |
| | | | | | 51 | Kichemchem |
| | | | | | 52 | Kimalang'ombe |
| | | | | | 53 | Kidongo Chekundu |
| | | | 10 | Kisutu | 54 | Kisutu |
| | | | | | 55 | Mji Mpya |
| | | | | | 56 | Mianzini |
| | | | 11 | Makurunge | 57 | Mkwajuni |
| | | | | | 58 | Gezaulole |
| | | | | | 59 | Kifude |
| | | | | | 60 | Kitame |

SEHEMU E.

(Mipaka ya eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo)

Mpaka unaanza katika nukta BV714(VP608) (E 503603 N 9268218), kisha unaelekea hadi nukta BPA74 (E 506125 N 9267384), kisha mpaka unafuata hadi nukta BP8, BP9 na VP610 (E 507453 N 9266940). Baada ya hapo, mpaka unakutana na Mto Mpiji na unafuata mwelekeo wa Kusini Mashariki wa Mto Mpiji hadi pale unapovuka Barabara ya Bagamoyo. Kisha mpaka unafuata mwelekeo wa Mto Mpiji hadi unapoingia Bahari ya Hindi. Mpaka unafuata mwambao wa Bahari ya Hindi kupitia vitongoji vya Kiharaka, Mapinga na Kerege hadi pale ambapo Mto Mkuza unaingia Bahari ya Hindi. Kisha mpaka unaendelea kufuata mwambao wa Bahari ya Hindi kupitia vitongoji vya Kondo, Mlingotini na Pande hadi pale ambapo Mto Pimbini unaingia Bahari ya

*Tangazo la Serikali Na.603 (Linaendelea.)*

Hindi. Mpaka unafuata mwambao wa Bahari ya Hindi hadi nukta VP617 (E 495146 N 9285691), kisha unafuata mwambao wa Bahari ya Hindi kwa mwelekeo wa Kaskazini Magharibi hadi pale ambapo Mto Ruvu unaingia Bahari ya Hindi. Mpaka unaendelea kufuata mwambao wa Bahari ya Hindi kuelekea Kaskazini hadi pale ambapo Mto Wami unaingia Bahari ya Hindi. Mpaka unafuata mwelekeo wa Mto Wami hadi pale unapoanza kukutana na reli ya Tanga, kisha unafuata mwelekeo wa reli kupitia nukta ZC527, ZBS924 hadi nukta ZEM1 (E 470170 N 9305857). Baada ya hapo, mpaka unafuata nukta ZEM2, ZEM3, ZEM4 hadi ZEM5 (E 463803 N 9306118), inayotenganisha mpaka wa kijiji kati ya Fukayosi na Matipwili. Kisha mpaka unapita kupitia nukta BV236 hadi nukta VP684 (E 464434 N 9308598), ambapo mpaka unaelekea hadi pale unapokutana na Mto Wami. Mpaka unafuata mwelekeo wa Mto Wami hadi nukta VB103 (E 462341 N 9307222), kisha unapita kupitia nukta BV758, VB102, VB749 hadi nukta BV340 (E 458659 N 93001361). Baada ya hapo, mpaka unaelekea kwenye nukta BV337, VB109, hadi pale unapokutana na barabara ya Msata. Mpaka unapita kupitia VP122 hadi nukta BV251 (E 454743 N 9293220), ambapo vijiji vya Mwavi, Kiwangwa na Bago vinakutana. Baada ya hapo, mpaka unaelekea nukta VB108 na kwenda hadi nukta VP678 (E 453382 N 9291134), ambapo unakutana na Mto Magongoni. Mpaka unafuata mwelekeo wa Mto Magongoni kupitia nukta BV180 (E 454433 N 9290714), kisha unapita kupitia nukta BV181, VP689, BV182 hadi nukta BV206 (E 457777 N 9287358), ambapo vijiji vya Fukayosi, Mwavi, Msinune na Mkenge vinakutana. Mpaka unaendelea kuelekea nukta BV207, BV203, BV204, BV205 hadi nukta BV197 (E 463732 N 9278348), kisha unapita kupitia nukta BV215 hadi nukta BV216 (E 467911 N 9275504). Mpaka unaelekea umbali wa kilomita 8 hadi nukta VP560 (E 471372 N 9282768), kisha unaelekea Kusini Mashariki hadi nukta BV669 (E 476060 N 9277486). Baada ya hapo, mpaka unaelekea upande wa Mashariki hadi nukta NP856 (E 478793 N 9278202), kisha mpaka unapita kupitia nukta BV706 hadi nukta NP (E 479802 N 9278104), ambapo unakutana na Mto Ruvu. Mpaka unafuata mwelekeo wa Kusini wa Mto Ruvu hadi pale unapokutana na Mto Chatota, ambapo unafuata mwelekeo wa Mto Chatota hadi nukta FDI (E 479516 N 9271160). Mpaka unapita kupitia nukta FD2, FD3, hadi nukta FD4 (E 482674 N 9270419), kisha unaelekea nukta FD5 (E 48482534 N 9268138). Mpaka unafuata mwelekeo wa Mashariki hadi nukta FD6 (E 485417 N 9268234). Mpaka unapita kupitia nukta FD7 hadi nukta FD8 (E 485540 N 9270148), kisha unafuata mwelekeo hadi nukta FD (E 487523 N 9271198). Baada ya hapo, mpaka unaelekea nukta BV132 (E 487418 N 9271292), ambapo unakutana na Mto Chambe. Mpaka unapita kupitia nukta FD11, FD12, hadi nukta VP665 (E 493064 N 9276495), kisha mpaka unaelekea nukta VP664 (E 496457 N 9275957). Mpaka unaendelea kupitia nukta VP661, FR17, VP662, VP663 hadi nukta VP657 (E 500459 N 9274094), ambapo unakutana na Mto Mkuza. Kisha mpaka unafuata mwelekeo wa Kusini wa Mto Mkuza hadi nukta NPB (E 500265 N 9267702), kisha mpaka unaelekea nukta VP656 (E 502451 N 9268905). Hatimaye, mpaka unarudi kwenye nukta ya mwanzo ya BV714(VP608) (E 503603 N 9268218).

Dodoma,
29 Agosti, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*